JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na** HW/A.10/48/ VOL. I/158 21/08/2025

**TANGAZO LA NAFASI AROBAINI (40) YA KAZI ZA MUDA WA MIEZI MINNE YA WAKUSANYA MAPATO.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi anatangaza nafasi Arobaini(40) za kazi ya Mkataba ya wakusanyaji mapato(revenue collectors) ambao wataajiriwa kwa muda wa miezi minne(4) kuanzia Tarehe 1 Septemba, hadi Tarehe 30, Disemba 2025 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Mapato hayo yatakusanywa katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama vitakavyoonekana kwenye Mikataba itakayoandaliwa baada ya taratibu za ajira ya muda kukamilika.

**MAJUKUMU YA KAZI.**

1. Kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vya mapato atakavyopangiwa.
2. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yaliyokusanywa kwa siku hiyo yanawekwa Benki.
3. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yanakusanywa kwa kutumia mashine ya kukusanyia mapato (POS MACHINE) na kutoa stakabadhi halali za Halmashauri.
4. Kuhakikisha kuwa mashine ya kukusanyia mapato (POS MACHINE) inakuwa katika hali ya usalama na inatumika muda wote bila kuzimwa (inakuwa ONLINE).
5. Kuhakikisha kuwa mteja anapata risiti yake ya ushuru/tozo aliolipia kwa wakati pasipo kuchukua pesa mkononi bila kutoa risiti.
6. Kufanya kazi yoyote inayohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa mapato utakayopangiwa na msimamizi wa kazi na mahali popote katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

## MALIPO

Malipo kwa kazi hii ni asilimia 10% ya makusanyo yatakayokusanywa na kuwekwa benki na mkusanya mapato katika chanzo husika kwa kila mwezi.

**SIFA MUHIMU ZA WAOMBAJI:**

1. Awe raia wa Tanzania ambaye ni mkazi wa Halmashauri ya Bahi.
2. Awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA).
3. Awe amehitimu kidato cha nne na kuendelea.
4. Awe na ujuzi wa kutumia kwa ufasaha simu janja (smart phone) au Pos.
5. Mwombaji anatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika katika maeneo wanayotoka na aliye tayari kuchukuliwa mali zake bila masharti yeyote mwombaji akiajiriwa endapo atapatikana na upotevu wa pesa za mwajiri
6. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha picha mbili (passport size) za rangi za hivi karibuni.
7. Mwombaji atakayekidhi sifa zinazotakiwa ataajiriwa na kupangwa kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya mapato vya Halmashauri ya Bahi
8. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na viambatanisho vinavyohitajika kama vile vivuli vya vyeti vyake vya elimu, NIDA na zitumwe kwa Anwani.

**MASHARTI KWA WAOMBAJI WA AJIRA HII:**

i. Awe na Kitambulisho cha Taifa(NIDA)
ii. Awe na umri wa miaka 18 hadi 45
iii. Awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha lugha ya kingereza au Kiswahili
iv. Awe mwaminifu, mwadilifu, na mwenye weledi
v. Awe hajawai kupatikana na hatia kwa makosa ya jinai
vi. Mwombaji asiwe na deni lolote Halmashauri ya Bahi katika mifumo yote miwili(TAUSI na LGRCIS) kwa wakusanya mapato waliowai kufanya kazi na Halmashauri ya Bahi
vii. Barua ya maombi ipitie kwa Mtendaji wa Kijiji.
viii. Barua ya maombi iwe na namba za simu na anwani ya kuaminika.
ix. Majina kamili ya wadhamini na namba zao za simu zinazopatikana.



CamScanner

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA BAHI,**
**S.L.P 2993**
**DODOMA.**

Maombi yanapokelewa kuanzia **Tarehe 22/08/2025 hadi 01/09/2025 saa 9:00 Alasili,** Katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya BAHI

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI**

Albina W. Mtumbuka
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**BAHI**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI



CamScanner